# 4

# Mbinu ya Uwezeshaji katika Mitaala ya Kiswahili na Ufundishaji wake katika Vyuo Vikuu

Carren NYANDIBA

## Utangulizi

Makala hii inajadili hali ya ufundishaji wa Kiswahili kutokana na maendeleo na mabadiliko kama vile usasa, utandawazi, uhamiaji na maingiliano ya watu. Hali hii inahitaji mpangilio mpya wa Mtaala wa elimu ya Kiswahili. Kote ulimwenguni kuna haja ya mwelekeo mpya wa kiisimu ambao unahitaji mabadiliko katika mitaala ya elimu ya lugha. Msingi wa aina hii ya mabadiliko ni matumizi ya ufundishaji unaotambua uwezo wa mwanafunzi. Lengo kuu la mafunzo yaliyokitwa kwenye uwezo ni kuwaandaa wanafunzi wanaoweza kubadilika na kukubali mabadiliko, ambao wanaweza kudhihirisha uwezo wao katika hali changamano zisizotarajiwa watakazokumbana nazo katika maisha yao ya kijamii na kitaaluma

Makala inachunguza namna mbinu ya uwezeshaji inavyoweza kutumika katika maandalizi na ufundishaji wa mitaala ya Kiswahili katika vyuo vikuu vya Afrika Mashariki. Mbinu ya uwezeshaji inampa mwanafunzi uhuru mkubwa zaidi ya mwalimu katika ujifunzaji. Hoja kuu katika makala hii ni kwamba mtaala unaoandaliwa kwa kumwezesha mwanafunzi huwa unamsaidia kujifunza mikakati ya kujifunza mwenyewe na kujiendeleza ipasavyo. Mbali na uhuru wa kujifunza, mwanafunzi anawezeshwa kuwajibika katika

# 4

# Mbinu ya Uwezeshaji katika Mitaala ya Kiswahili na Ufundishaji wake katika Vyuo Vikuu

Carren NYANDIBA

## Utangulizi

Makala hii inajadili hali ya ufundishaji wa Kiswahili kutokana na maendeleo na mabadiliko kama vile usasa, utandawazi, uhamiaji na maingiliano ya watu. Hali hii inahitaji mpangilio mpya wa Mtaala wa elimu ya Kiswahili. Kote ulimwenguni kuna haja ya mwelekeo mpya wa kiisimu ambao unahitaji mabadiliko katika mitaala ya elimu ya lugha. Msingi wa aina hii ya mabadiliko ni matumizi ya ufundishaji unaotambua uwezo wa mwanafunzi. Lengo kuu la mafunzo yaliyokitwa kwenye uwezo ni kuwaandaa wanafunzi wanaoweza kubadilika na kukubali mabadiliko, ambao wanaweza kudhihirisha uwezo wao katika hali changamano zisizotarajiwa watakazokumbana nazo katika maisha yao ya kijamii na kitaaluma

Makala inachunguza namna mbinu ya uwezeshaji inavyoweza kutumika katika maandalizi na ufundishaji wa mitaala ya Kiswahili katika vyuo vikuu vya Afrika Mashariki. Mbinu ya uwezeshaji inampa mwanafunzi uhuru mkubwa zaidi ya mwalimu katika ujifunzaji. Hoja kuu katika makala hii ni kwamba mtaala unaoandaliwa kwa kumwezesha mwanafunzi huwa unamsaidia kujifunza mikakati ya kujifunza mwenyewe na kujiendeleza ipasavyo. Mbali na uhuru wa kujifunza, mwanafunzi anawezeshwa kuwajibika katika

ujifunzaji. Uhuru na uwajibikaji ni nguzo muhimu za elimu ya chuo kikuu.

Makala inahimiza haja ya mtaala wa Kiswahili kuandaliwa kwa njia ambayo inamwezesha mwanafunzi kujifanyia shughuli za kiutafiti na kuwasilisha matokeo yake kupitia makala na ripoti zinazozingatia mahitaji ya kimsingi ya viwango vya kitaaluma. Kozi za vyuo vikuu zinahitaji mwanafunzi ajifanyie utafiti mpana nyanjani zaidi ya yale anayofunzwa katika mihadhara. Ili hili lifanyike, mwanafunzi anahitaji kuwa huru na kuwajibika. Mwanafunzi anastahili kuandaliwa kujitegemea, kujituma, kuwajibika na kujielekeza. Kozi inafaa kuhakikisha kwamba mwalimu na mwanafunzi wanapewa nafasi zao na kuelewa majukumu ya kila mmoja, hasa kwa kuzingatia malengo na mahitaji ya mwanafunzi. Mtaala ndio huonyesha kinachostahili kufundishwa na kuelekeza ufundishaji.

## Mitaala na Elimu katika Jamii

Mtaala ni mwongozo wa elimu. Mtaala huonyesha kile ambacho jamii inatarajia wanafunzi kufundishwa wakati wanapoandaliwa kuchukua nafasi za kuiendeleza jamii kupitia utekelezwaji wa majukumu mbalimbali. Mtaala si tukio la kisadfa. Hirst (1974) anapambanua hoja hii kwa kueleza kwamba kila mtaala una madhumuni; na kila mtaala una matarajio na shughuli za kuyafanikisha matarajio hayo. Hivyo, madhumuni huundwa kwa ajili ya kumwelekeza Mwalimu, nazo shughuli huandaliwa ili zitekelezwe. Haya yote yana maana kwamba mtaala ni jambo la kimaksudi ambalo huchukua muda na ujuzi kuandaa.

Kwa ujumla, wananadharia wameainisha mitaala mikuu mitatu kutegemea madhumuni na matarajio yake. Hii ni: Mtaala wa Kimaudhui; Mtaala wa Kiufundishaji; na Mtaala wa Kiujifunzaji. Kuna tofauti ndogondogo baina ya mitaala hii.

ujifunzaji. Uhuru na uwajibikaji ni nguzo muhimu za elimu ya chuo kikuu.

Makala inahimiza haja ya mtaala wa Kiswahili kuandaliwa kwa njia ambayo inamwezesha mwanafunzi kujifanyia shughuli za kiutafiti na kuwasilisha matokeo yake kupitia makala na ripoti zinazozingatia mahitaji ya kimsingi ya viwango vya kitaaluma. Kozi za vyuo vikuu zinahitaji mwanafunzi ajifanyie utafiti mpana nyanjani zaidi ya yale anayofunzwa katika mihadhara. Ili hili lifanyike, mwanafunzi anahitaji kuwa huru na kuwajibika. Mwanafunzi anastahili kuandaliwa kujitegemea, kujituma, kuwajibika na kujielekeza. Kozi inafaa kuhakikisha kwamba mwalimu na mwanafunzi wanapewa nafasi zao na kuelewa majukumu ya kila mmoja, hasa kwa kuzingatia malengo na mahitaji ya mwanafunzi. Mtaala ndio huonyesha kinachostahili kufundishwa na kuelekeza ufundishaji.

## Mitaala na Elimu katika Jamii

Mtaala ni mwongozo wa elimu. Mtaala huonyesha kile ambacho jamii inatarajia wanafunzi kufundishwa wakati wanapoandaliwa kuchukua nafasi za kuiendeleza jamii kupitia utekelezwaji wa majukumu mbalimbali. Mtaala si tukio la kisadfa. Hirst (1974) anapambanua hoja hii kwa kueleza kwamba kila mtaala una madhumuni; na kila mtaala una matarajio na shughuli za kuyafanikisha matarajio hayo. Hivyo, madhumuni huundwa kwa ajili ya kumwelekeza Mwalimu, nazo shughuli huandaliwa ili zitekelezwe. Haya yote yana maana kwamba mtaala ni jambo la kimaksudi ambalo huchukua muda na ujuzi kuandaa.

Kwa ujumla, wananadharia wameainisha mitaala mikuu mitatu kutegemea madhumuni na matarajio yake. Hii ni: Mtaala wa Kimaudhui; Mtaala wa Kiufundishaji; na Mtaala wa Kiujifunzaji. Kuna tofauti ndogondogo baina ya mitaala hii.

Mtaala wa Kimaudhui huundwa kwa kusisitiza masomo au kozi kuu za kimsingi zinazohitajika katika jamii. Kwa baadhi ya wachunguzi, mtaala wa aina hii huendeleza tofati za kijamii kwa kuwa aghalabu hufundisha kozi ambazo makundi fulani ya kijamii yanazipendelea. Kwa watu wengine, mtaala huu ni msingi mzuri wa kujenga usawa wa kijamii kwa kufundisha masomo kwa wanafunzi wote bila ubaguzi. Kwa ujumla, Mtaala wa Kimaudhui hutumiwa kuwachuja na kuwateua wale wanaopata fursa ya kujiendeleza kitaaluma. Kwa kuwa ni idadi ndogo ya wanafunzi wanaoendeleza masomo hadi ngazi ya juu, basi mtaala huu unaweza kulaumiwa kuwa unawabagua baadhi ya wanafunzi.

Kwa upande mwingine, kuna maoni kwamba mtaala mzuri ni ule ambao unawaanda wanafunzi kwa majukumu ya ujenzi wa taifa. Hii ina maana kwamba kila kinachofundishwa kiweze kuwa na umuhimu wa kimatumizi baadaye. Masomo yapangwe ili yafundishe stadi zinazohitajika kufanya kazi. Hivyo basi, mada zinazofundishwa, malengo ya ufundishaji, namna ya kufundisha, na hata tathmini ihusiane na ujifunzaji wa stadi muhimu katika utendaji kazi baadaye. Katika hali hii, mtaala unapangwa na serikali kuwa chombo cha kuwaandaa watumishi wa baadaye wenye stadi za kufanikisha maendeleo ya kitaifa.

## Uwezeshaji wa Mwanafunzi na Ujifunzaji

Dhana ya uwezeshaji imetumika sana kumrejelea mwanafunzi akiwa darasani. Hata hivyo, katika Makala hii, dhana hii inatumika kwa maana pana zaidi ya uwezeshwaji unaotokea katika chuo kikuu ndani na nje ya darasa. Uwezeshwaji unahusisha ujifunzaji katika mazingira mapana ya chuo kikuu na hata nje yake. Ni ujifunzaji ambao mwanafunzi anajituma na kutekeleza popote pale kwa minajili ya kufanikisha kozi anayojifunza.

Hivyo basi, makala hii inasisitiza haja ya kuwa na mtaala unaotambua kwamba mwanafunzi hajifunzi tu darasani pekee, bali hupata maarifa anayoyahitaji katika jamii pana zaidi ya chuo kikuu. Ni kutokana na kutambua umuhimu wa ulimwengu nje ya chuo kikuu kama darasa la mwanafunzi wa chuo kikuu ambapo makala inaonelea umuhimu wa mitaala ya Kiswahili kufanyiwa marekebisho ili ikidhi mahitaji hayo, ikiwa ni pamoja na kumwandaa mwanafunzi kujifunza kuwa huru na kuutumia uhuru huo kwa nidhamu na kwa kuwajibika.

Kwa takribani miongo saba sasa, nadharia zimeonyesha nia na haja ya kufanya mabadiliko makubwa katika mitaala ya elimu ya lugha. Tofauti na ilivyokuwa katika kipindi cha awali cha maendeleo ya isimu na lugha, na tangu kuibuka kwa Mkabala wa Kimawasiliano mwisho wa mwongo wa 1970 na mwanzo wa mwongo wa 1980, ufundishaji hautawaliwi na kanuni za lugha, badala yake mkazo sasa uko kwa maana itokanayo na lugha kama mfumo wa mawasiliano (taz. Nunan na Lamb, 1996 na Richards na Rodgers, 1986).

Mielekeo katika nadharia ya lugha na ufundishaji wake imeweka haja ya kutafakari dhima na majukumu ya wahusika katika mchakato huo. Miongoni mwa wahusika wakuu katika ufundishaji wa lugha ni wanafunzi. Hii ndiyo sababu kuu ya kutilia mkazo haja ya kuwa na mitaala ya Kiswahili inayolenga kumpa mwanafunzi uhuru lakini wakati huohuo kumfanya awajibike.

Tangu kuanzishwa, na katika maendeleo yake, Mstakabali wa Kimawasiliano unaangazia mwanafunzi, mwalimu, mada na vifaa vya ufundishaji lugha. Tofauti na mikabala ya awali ambayo iliwachukulia wanafunzi kuwa watazamaji na wasikilizaji tu, Mkabala wa Kimawasiliano unamweka mwanafunzi katika nafasi kubwa ya kuwa mshiriki kikamilifu katika hatua mbalimbali za mchakato wa ufundishaji. Umuhimu wa mwalimu unathaminiwa kufanikisha mawasiliano na siyo kutawala shughuli nzima ya ujifunzaji. Mada na mitaala nayo inahitajika iundwe kwa

namna ambayo itawezesha matumizi ya lugha katika hali halisi ya kijamii. Katika hali hizi zote, mwanafunzi anastahili kupewa kipaumbele. Hii ndiyo sababu ya kusisitiza umuhimu wa mbinu ya uwezeshaji wa nafasi hii muhimu ya mwanafunzi katika kujifunza lugha.

Kutokana na maendeleo katika Mkabala wa Kimawasiliano, utafiti umekuwa ukifanywa na kuonyesha haja ya kumzingatia mwanafunzi zaidi ya mwalimu na mada anayojifunza. Mbali na mwanafunzi, pana umuhimu pia wa kutathmini mazingira anamojifunzia mwanafunzi. Wanafunzi wamejitokeza kuwa muhimu katika kuelekeza maandalizi, utekelezaji na tathmini ya mitaala ya elimu ya lugha. Inatarajiwa kwamba habari za kumzingatia mwanafunzi zitawekwa katika kila awamu na hatua ya mtaala. Kwa namna hii, uandaji wa mitaala inakuwa shughuli inayowashirikisha wahusika wote ikiwa ni pamoja na wanafunzi. Hii ni tofauti kabisa na ilivyokuwa zamani ambapo wanafunzi hawakushirikishwa kikamilifu katika maandalizi na utekelezaji wa mtaala (Nunan, 1989).

Dickinson (1987: 9) anafafanua mabadiliko yaliyotokea katika juhudi za uwezeshaji wa wanafunzi katika ujifunzaji. Kutokana na maendeleo ya nadharia ya lugha na ujifunzaji, mchakato wa kuandaa mtalaa unatilia mkazo majukumu na wajibu wa mwanafunzi. Ujifunzaji unaeleweka sasa kuwa juhudi za mwanafunzi binafsi. Hata ingawa kuna wahusika na mahitaji mengine, ufanisi wa ujifunzaji unamtegemea mwanafunzi: awajibike katika mipaka ya uhuru alionao. Lakini kwa kuwa suala la uwajibikaji ni gumu kutekelezwa, mwanafunzi anatarajiwa kuwa na sifa maalumu za kimsingi ambazo zitafanikisha ujifunzaji kwenye mazingira huru ndani na nje ya darasa la chuo kikuu. Hii ndiyo sababu kuu muhimu ya kumwandaa mwanafunzi awezeshwe kuwajibika kujifunza.

Hivyo basi, Tudor (1996:34) anadai kwamba mbinu ya kumwezesha mwanafunzi inahitaji kusisitiza haja ya

kujitambua ili mwanafunzi aandaliwe kutambua na kufahamu umuhimu wa mchakato wa ujifunzaji lugha na kujiweka tayari kujituma na kushiriki kikamilifu katika shughuli hiyo. Ili kumsaidia mwanafunzi kujenga uwezo wa kuwajibika katika ujifunzaji, mtaala hauna budi kuchunguzwa na kuzingatiwa kwa makini. Mtaala umsaidie mwanafunzi kujituma na kuelewa kwa kina suala zima la ujifunzaji lugha, na kumwelekeza namna ya kupata maarifa na stadi zinazohitajika ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Kutokana na umuhimu wa kumshirikisha mwanafunzi katika ujifunzaji, Nunan (1986: 132) anatoa sifa zifaazo kuzingatiwa katika somo au kipindi cha lugha:

i. Mada zipatikane kutoka mazingira halisi;
ii. Wanafunzi washirikishwe kikamilifu katika kujifunza na kutafuta majibu ya maswali wanayokumbana nayo;
iii. Shughuli za ujifunzaji lugha zihusiane na mahitaji ya kimawasiliano;
iv. Wanafunzi waruhusiwe kuamua wanachotaka kujifunza, namna ya kujifunza na wakati wa kujifunza;
v. Wanafunzi wawe huru kujenga uhalisia wa ulimwenguni ndani mwa madarasa yao;
vi. Wanafunzi na walimu wao watekeleze majukumu mbalimbali ya ujifunzaji ndani na nje ya madarasa;
vii. Wanafunzi wawezeshwe kutambua lugha kama mfumo wa mawasiliano;
viii. Wanafunzi wahimizwe kuendeleza stadi za ujifunzaji;
ix. Stadi nne kuu za mawasiliano (kusikiliza; kuongea; kusoma; kuandika) zisetwe;
x. Stadi nne ndogo za mawasiliano (sarufi; msamiati; matamshi; mwendelezo) zitumike;

xi. Wanafunzi washirikishwe katika matumizi ya lugha kiubunifu.

## Mtaala wa Uwezeshaji wa Mwanafunzi katika Ujifunzaji wa Lugha

Katika miaka ya hivi karibuni, nchi nyingi ulimwenguni zimeanza kutilia mkazo uundwaji wa mtaala unaomzingatia mwanafunzi katika ujifunzaji. Mabadiliko hayo kwenye ujifunzaji yanatokana na maendeleo ya kijamii na haja ya kukidhi mahitaji ya binadamu. Bila kujali asili na maendeleo hayo, mbinu za uwezeshaji zinasisitiza haja ya kuhakikisha kwamba elimu inayotolewa kupitia masomo mbalimbali inampa mwanafunzi fursa ya kujenga ari ya kutaka kujigundulia mambo, kujiongezea maarifa, kuwa mbunifu, kufahamu anachojifunza, na kujifunza kwa vitendo badala ya kumaizi na kukariri mambo tu (Díaz-Barriga, 2015).

Hali za maendeleo na mabadiliko zinawalazimu wahusika wote kuifanyia marekebisho mitaala katika viwango vyote vya elimu, ikiwamo ile ya vyuo vikuu. Maisha yanabadilika na mada za elimu nazo hazina budi kufanyiwa mageuzi. Mazingira ya elimu nayo yanabadilika kila wakati. Vilevile, kutanuka kwa TEHAMA kuna athari kubwa kwa mfumo wa elimu kote ulimwenguni. Mitandao ya kijamii hasa miongoni mwa vijana ina maana kwamba haja ipo ya kuhakikisha wanapewa elimu yenye maana kwao na maisha yao ya baadaye. Isitoshe, jamii pana nayo inapitia mabadiliko makubwa. Kinachotolewa kupitia elimu hakina budi kuakisi hali halisi iliyoko nje ya madarasa ya ujifunzaji.

Hivyo basi, nadharia kuhusu maana ya mtaala, utekelezaji na tathmini yake zinahitaji kufikiriwa upya kwa mujibu wa uhalisi wa jamii ya sasa. Pana umuhimu wa kutafakari kuhusu majukumu ya mtaala muafaka unaokidhi mahitaji ya ulimwengu wa sasa wenye mabadiliko makubwa ya mara kwa mara. Katika kufanya hivyo, ni muhimu

kukumbuka mahitaji ya mwanafunzi na nafasi yake ya kujifunza kwa vitendo. Mtaala mpya umpe fursa ya kuijtambua na kujieleza; siyo kufundishwa mambo ambayo hayana uhusiano na maisha.

Kwa muda mrefu sasa, mitaala katika vyuo vikuu imekuwa ikiundwa na kutekelezwa bila kuwazingatia walengwa ambao ni wanafunzi. Siyo tu wanafunzi hawana fursa kishiriki kikamilifu, lakini pia mazingira wanamofundishiwa yana changamoto zake. Walimu ndio huamua nini cha kufundisha na lini na wapi mafundisho yatatolewa. Hali hii si muafaka kwa ujifunzaji unaostahili. Mtaala unaomjali mwanafunzi unahitaji kuwashirikisha kikamilifu katika maandalizi na utekelezaji wake. Usiwe mtaala uliofumwa kwa namna hauwezi kufanyiwa marekebisho na kuimarishwa. Hii haina maana kwamba walimu hawatambuliwi. La hasha! Walimu ni wataalamu ambao wameandaliwa na wanatarajiwa kuchangia katika kupitisha maarifa kwa wanafunzi. Hata hivyo, jukumu lao liwe la kufanikisha tu, lisiwe la kuwapuuza wanafunzi.

Maendeleo ya TEHAMA yana maana kwamba mitaala mizuri ni ile ambayo itawapa wanafunzi fursa ya kujifunza wenyewe kupitia mitandao mbalimbali. Wanafunzi waweze kuwasiliana na wenzao na washirikiane katika ujifunzaji. Hali hizi zinamaanisha kwamba mtaala hauwezi kuandaliwa bila kumjali mwanafunzi na mazingira.

## Mbinu ya Uwezeshaji katika Ujifunzaji wa Kiswahili katika Vyuo Vikuu

Mtaala wa Kiswahili katika vyuo vikuu unatarajiwa kuwa na sifa ambazo zinamwezesha Mwalimu kukabiliana na ukuaji na mabadiliko ya jamii, ikiwa ni pamoja na wanafunzi, wanachojifunza na matarajio yao. Miongoni mwa mambo ya kimsingi kuzingatiwa ni uhuru wa mwanafunzi kujifunza Kiswahili. Hii ina maana kwamba mitaala iliyopo inahitaji

kuchunguzwa na kuhakikisha kwamba inamzingatia mwanafunzi na kumpa nafasi ya kujiendeleza kitaaluma. Wanafunzi wa Kiswahili wawezeshwe kupitia kozi mbalimbali kuyaelewa mazingira wanamokulia na namna ya kuishi kwa mafanikio katika shughuli mbalimbali wanazozifanya.

Hivyo basi, hatua zinazohitajika ni kuhakikisha mitaala iliyopo inafanyiwa mabadiliko na kuanzisha kozi zitakazowapa wanafunzi uhuru na uwezo wa kubuni mambo. Ubunifu utakuwa msingi wa ujifunzaji unaoelekezwa kwenye malengo ya maendeleo ya mwanafunzi binafsi na kwa jamii pana. Cullen, n.w (2012) wanasema licha ya uzingatiaji wa uhuru wa mwanafunzi, mwalimu bado ana umuhimu mkubwa wa kumwelekeza ili kufanikisha ujifunzaji. Elimu inayotolewa kupitia mtaala huo iwe ya kujifunza kwa vitendo na inayonufaika na hali halisi katika mazingira ya wakati na mahali na inayomhitaji mwanafunzi kujitegemea zaidi kuliko kumtaka mwalimu kumfanyia takribani kila kitu. Kozi katika mitaala ya Kiswahili iundwe kwa kuzingatia mahitaji haya ya kimsingi. Kozi za Kiswahili zimlenge mwanafunzi na wajibu wake katika jamii.

Mitaala ya Kiswahili inakabiliana na changamoto za kuhakikisha kwamba inatimiza mahitaji ya jamii inayokua kwa haraka na yenye mahitaji makubwa na mengi. Baadhi ya mambo yasiyoweza kupuuzwa ni haja ya kuandaa kozi mbalimbali zilizo na uwezo wa kuishughulikia jamii kikamilifu. Siyo tu suala la wingi wa kozi, bali pia uchipukaji wa nadharia za lugha na ujifunzaji, pamoja na mbinu na vifaa vinavyohitajika kufanikisha hilo. Mitaala ya Kiswahili inastahili kuwa na kozi ambazo zinamwelimisha mwanafunzi kuhusu uhuru wake binafsi na wajibu wake katika kuiendeleza jamii ya Afrika Mashariki.

Elimu yoyote ile imwezeshe mwanafunzi kuishi katika jamii ya kisasa yenye mabadiliko makubwa. Jamii hiyo haina namna moja ya kuona na kufanya mambo; kuna mitazamo

mbalimbali na jinsi za kukamilisha shughuli; kuna maoni ya watu na makundi tofautitofauti yenye umuhimu; na kuna maingiliano na mitagusano ya watu wanapoendesha shughuli zao. Elimu nzuri ni ile inayotambua wingi huo: wa watu, maoni, mitazamo, matarajio na mielekeo. Mitaala ya Kiswahili isiwe ya aina moja katika kila Nchi Mwanachama wa Jumuiya ya Afrika. Vyuo vikuu mbalimbali viandae kozi za Kiswahili ambazo zitawezesha wanafunzi kujifunza kuhusu hali halisi za jamii zao na Jumuiya ya Afrika Mashariki, pamoja na historia na maendeleo yake. Maana na umuhimu wa utangamano na maendeleo endelevu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ni mambo yanayoweza kufundishwa kupitia kozi bunifu.

Weimer (2013) anaonyesha kuwa kozi za vyuo vikuu zinaweza na zinahitaji kufanyiwa marekebisho ili kukidhi mahitaji ya kijamii. Katika taaluma, mahitaji hayo yanadhihirika kupitia nadharia mbalimbali. Marekebisho yanoyafanywa yamlenge mwanafunzi na kumpa uhuru na uwezo wa ujifunzaji. Vivyo hivyo, kozi za Kiswahili katika vyuo vikuu vya Afrika Mashariki zifanyiwe marekebisho kiubunifu zaidi ya vile ambavyo imefanyika mpaka sasa. Tofauti zionekane katika mitaala ya vyuo vikuu mbalimbali, badala ya kuonekana kozi zilezile wakati wote. Mitaala ya Kiswahili ijengwe kwa nadharia, ambazo nazo zinakua na kubadilika. Na muhimu zaidi, mwalimu atekeleze wajibu wake wa kumwelekeza tu mwanafunzi ambaye ndiye mlengwa mkuu.

McCombs na Whisler (1997) na McCombs na Vakili (2005) wamejadili misingi mikuu ambayo inaweza kusaidia wakati wa kufanyia marekebisho mtaala wa elimu. Ni muhimu kutambua kwamba hawa wataalamu wanasisitiza haja ya kutambua elimu kuwa mchakato unaoendelea katika maisha ya mwanadamu na siyo tukio la kipindi maalumu tu. Aidha, elimu ni uimarishwaji wa maarifa katika mazingira tofautitofauti na siyo tu darasani. Ni katika mantiki hii ambapo elimu na mtaala wake unafaa kuzingatia mwanafunzi mno na kutilia maanani

mchakato kuliko mambo mengine. Hivyo basi, mapendekezo ya kufanyia marekebisho mtaala wowote wa elimu usisitize mihimi hiyo: mwanafunzi na mchakato.

Kwanza, Mtaala unaundwa kwa ajili ya kumwezesha mwanafunzi kujifunza. Hivyo, uundwaji wa mtaala unastahili kumwelewa mwanafunzi na uzoefu alionao, maoni aliyonayo, matarajio yake, mahitaji yake, na jinsi anavyotaka kujifunza. Kwa mitaala ya Kiswahili katika vyuo vikuu vya Afrika Mashariki, mambo haya ni ya kimsingi. Kwa kuwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ni tofauti kihistoria na kimaendeleo, mitaala ya Kiswahili idhihirishe hali hizo katika kozi zake mbalimbali.

Pili, marekebisho kwa mtaala wa elimu yachunguze hali ya mchakato mzima wa ujifunzaji. Marekebisho ya mtaala yafanywe kwa kuzingatia maendeleo ya taaluma na nadharia za ukuaji wake. Utafiti ni msingi mzuri wa kukadiria maendeleo katika taaluma. Matokeo ya utafiti yatabainisha sababu za watu kutaka kujifunza na namna mafundisho yanavyopatikana. Kuna sababu za watu kujifunza na haja ya kutilia mkazo nafasi ya mwanafunzi katika maandalizi ya mtaala. Kumzingatia mwanafunzi katika mtaala ni kumpa uhuru wa kujiamulia mambo katika mchakato mzima wa ujifunzaji pamoja na miktadha mbalimbali ya kujifunza. Katika jamii ya sasa, wanafunzi wana uwezo wa kutumia TEHAMA kujiandalia wanachokitaka na kukitekeleza kwa namna wanavyotaka wenyewe. Hii ina maana kwamba wanafunzi wa sasa wana ubunifu wa hali ya juu sana wakilinganishwa na vipindi vilivyopita. Vivyo hivyo, mazingira na muktadha wa elimu umebadilika.

Mitaala ya Kiswahili katika vyuo vikuu vya Afrika Mashariki inufaike kutokana na matokeo ya utafiti katika taaluma za elimu, lugha na fasihi. Matokeo ya utafiti yanaweza kuwa yaliyofanywa na watafiti na wataalamu huku Afrika Mashariki au kwingineko duniani. Mitaala ya Kiswahili itakuwa na uhai na maana ikiwa imejengwa kwa misingi ya

usayansi na siyo mazoea tu. Lazima ieleweke kwa nini Kiswahili kinafundishwa na manufaa yake kwa mwanafunzi, nchi yake, Jumuiya ya Afrika Mashariki na kote duniani. Hivyo, kozi za Kiswahili ziundwe zinazoonyesha hali hizi mbalimbali. Isitoshe, umuhimu wa TEHAMA kama chachu ya maendeleo ya taaluma ya Kiswahili udhihirike katika kozi zinazoundwa.

Tatu, malengo ya ujifunzaji yanastahili kuzingatiwa wakati wa kufikiria mageuzi kwenye mtaala. Tofauti na ilivyokuwa zamani ambapo mtaala wa elimu ulitumiwa na mwalimu kudhihirisha umahiri wake, wakati wa maisha ya sasa yanayotawaliwa na utandawazi una mahitaji na matarajio yaliyobadilika sana. Mazingira ya elimu yamebadilika, na hivyo miktadha nayo imepata sura mpya. Maamuzi sasa hivi yanafanywa na kuchukuliwa na watu wengi. Kuna ubunifu wa kiwango cha juu na matarajio ya wahusika nayo ni mengi jinsi walivyo. Kwa mitaala ya Kiswahili, Mwalimu asitawale wanafunzi wake; awape uhuru na awaelekeze namna ya kuzitumia fursa wanazokutana nazo. Mahali na wakati wa kujifunza Kiswahili ni mambo yanayoamuliwa na sababu mbalimbali. Pasiwe na mtaala wa Kiswahili ambao utamfunga mwanafunzi asiweze kujifaragua na kujifunza taaluma hii namna anavyopenda mwenyewe.

Nne, ufumaji wa maarifa yanayolengwa kutolewa na kupatikana kupitia mtaala wa elimu. Hoja hii ina maana kwamba pana haja ya kuwa makini ili kufanikisha kuundwa kwa mtaala wenye mtiririko, mantiki na maana. Kwa kuwa wanafunzi ni wengi, matarajio yao pia yatakuwa mengi. Hivyo, haiwezekani mitaala ikaundwa kuzingatia mahitaji ya kila mwanafunzi. Kinachoweza kufanyika ni kwa mwalimu na Idara za Kiswahili kutathmini mahitaji ya jumla ya wanafunzi wao na kupendekeza kozi ambazo zitayazingatia kwa kiwango kikubwa. Wanafunzi wawezeshwe kushirikiana na kujifunza kwa pamoja ili kufanikisha malengo yao ya ujifunzaji.

Tano, marekebisho yasifanywe bila kufikiri kwa kina hali ya mwanafunzi na mazingira yake, pamoja na malengo ya jamii ya sasa na ya baadaye. Licha ya kwamba mwanafunzi anapewa uhuru mkubwa katika mbinu ya uwezeshaji, ni muhimu ifahamike kwamba hiyo haina maana mwalimu naye ametengwa katika mchakato wa elimu. Hapana. Mwalimu ni mtaalamu aliyeandaliwa kwa lengo la kufanikisha shughuli muhimu ya ujifunzaji. Kama asemavyo Weimer (2002) inapowezekana mwanafunzi na mwalimu wagawane madaraka katika kuandaa na kufanikisha mtaala wa elimu. Walimu wasiache majukumu yao ya kuwaongoza na kuwaelekeza wanafunzi. Kwa mitaala ya Kiswahili ya vyuo vikuu Afrika Mashariki, hali za wanafunzi pamoja na mazingira yao ni tofauti kwa kiasi kikubwa. Hivyo, tofauti hizi zionekane katika kozi, lakini pia pawe na kozi zinazojenga umoja wa kikanda. Walimu na wanafunzi washirikiane katika kufikiri kozi ambazo zinaweza kufanikisha malengo hayo ya jumla, bila kumtenga mhusika yeyote muhimu.

Hoja ya sita ambayo ni muhimu inahusu ukadiriaji wa viwango vya elimu inayotolewa pamoja na kutaka kujua mafanikio yanayopatikana. Mtaala wa elimu unahitajika kuhakikisha kile kinachoandaliwa kinastahili na kinazingatia viwango vya ubora. Hili linaweza kuonekana kupitia utekelezaji wa mtaala na ukadiriaji wa ujifunzaji. Mara nyingi hali hizi huweza kukadiriwa kupitia mitihani. Kwa bahati mbaya, wanafunzi huwa hawapendi mitihani kwa kuwa inawatia kiwewe na woga. Hali hii inakuwa mbaya zaidi pale alama zinatolewa na gredi kutumika kuwaweka wanafunzi katika viwango vya ufanisi. Wanafunzi wangependelea wajifunze tu bila kufanya mitihani. Lakini hali hii ikiruhusiwa itakuwa vigumu kujua kama malengo ya elimu na mtaala yametimizwa au la. Mrejesho ni muhimu kwa mwalimu na watawala katika ngazi mbalimbali za mfumo wa elimu. Hata hivyo, tatizo la mitihani linaweza kutatuliwa kwa kuutumia

kwa lengo la kuimarisha ujifunzaji na wala siyo kuonyesha matabaka kiutendaji.

**Hitimisho**

Makala hii imejadili umuhimu wa kumwezesha mwanafunzi kujifunza Kiswahili katika vyuo vikuu vya Afrika Mashariki. Kuna nadharia na mbinu mbalimbali za kufundisha lugha, na Kiswahili kinaweza kufaidi kutokana na matokeo ya utafiti ambao umefanywa na kuonyesha kuwa ujifunzaji ni bora zaidi katika kufanikisha malengo ya elimu. Elimu ina wajibu kwa nchi na kwa mwanafunzi. Hivyo, elimu inayotolewa ni muhimu kuzingatia hayo. Mwanafunzi wa Kiswahili anastahili kupewa nafasi muhimu katika mitaala ya vyuo vikuu.

Mitaala ya Kiswahili iliyoko kwenye vyuo vikuu inahitaji kufanyiwa marekebisho ili kukidhi maendeleo ya kijamii kwa jumla na ya kitaaluma. Marekebisho yafanywe kwa ubunifu unaozingatia wahusika mbalimbali pamoja na mahitaji yao. Vyuo vikuu vya Afrika Mashariki vina majukumu ya kitaifa, kikanda na kidunia. Kozi za Kiswahili zionyeshe namna vyuo vikuu vinazingatia mahitaji ya wanafunzi, nchi binafsi, ukanda wa Afrika Mashariki na ulimwengu kwa jumla. Mabadiliko na mageuzi kwenye mitaala yafanywe kwa kuzingatia nadharia za elimu na lugha. Kiswahili kitoe mchango kwa maendeleo ya taaluma hii. Mchango wa Kiswahili kwa taaluma ya elimu, lugha na fasihi uonekane kupitia utafiti na machapisho. Utafiti uwashirikishe wanafunzi katika kila hatua muhimu ya ujifunzaji wa Kiswahili.

**Marejeleo**


Cullen, R. Harris, M. na Hill, R. (2012) *The Leaner-Centred Curriculum: Design and Implementation.* Indiana: John Wiley and Sons

Dickinson, L. (1987). *Self-Instruction in Language Learning.* Cambridge: Cambridge University Press.

Hirst, P. (1974). *Knowledge and the Curriculum.* Oxford: Routledge and Kegan Paul.

McCombs, B. & Whisler, J.S. (1997). *The Learner-Centered Classroom and School. Strategies for Increasing Student Motivation and Achievement*. San Francisco: Jossey Bass.

McCombs, B. & Vakili, D. (2005). 'A Learner-Centered Framework for E-Learning' ktk *Teachers College Record*, 107(8), 1582-1600.

Nunan, D. (1989). *Designing Tasks for the Communicative Classroom.* Cambridge, UK: Cambridge University Press.

Richards, J.C. and Rodgers, T.S. (1986). *Approaches and Methods in Language Teaching.* Cambridge: Cambridge University Press.

Stern, H. H. (1983). *Fundamental Concepts of Language Teaching*. Oxford, England: Oxford University Press.

Tudor, I. (2006). "Trends in higher Education Language Policy in Europe: The Case of English as a Language of Instruction". Paper presented at the ECORE conference challenges in multilingual societies. June 9-10. Brussels- Belgium

Weimer, M. (2013). *Learner-Centered Teaching: Five Key Changes to Practice*. San Francisco: Jossey-Bass.

Weimer, M. (2002). *Learner-centered teaching: Five key changes to practice*. San Francisco, CA: John Wiley & Sons.